**ISSN 0856-034X**

***Supplement No. 7*** ***17th April, 2017***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 7 Vol. 98 dated 17th April, 2017*
Printed by the Government Printer Dar es Salaam by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 20 la tarehe 17/02/2017

SHERIA YA FEDHA SERIKALI ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MABANGO NA MATANGAZO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI ZA MWAKA 2017

Jina na Tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mabango na Matangazo) za Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi na zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo-

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

"Ada ya matangazo" maana yake ni tozo kwa mwombaji wa kibali kwa ajili ya kuruhusiwa kuweka bango au kutoa tangazo;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Bango la tangazo" maana yake ni kitu kilichotengenezwa au kujengwa kwa kutumia kifaa chochote kwa ajili ya kutolea au kuweka tangazo ambacho ukubwa wake utapimwa kwa futi za mraba;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi;

"Kibali" maana yake ni idhini ya maandishi itakayotolewa na Halmashauri ili kuruhusu kujenga au kuweka bango au kutoa matangazo ambayo itadumu kwa kadri ya muda utakavyoelekezwa na Halmashauri;

"Maeneo maalum" maana yake ni maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya Ofisi za Serikali, Taasisi au Mashirika ya umma, Mahakama, Hospitali na Vituo vya afya, Kambi za Jeshi na Polisi au maeneo mengine yanayohitaji utulivu wakati wote au maeneo mengine ambayo Halmashauri itaona inafaa kwa nyakati tofauti;

"Matangazo" maana yake ni taarifa zitakazotolewa kwa njia ya vipaza sauti, maandishi, picha au michoro itakayochorwa au kuandikwa au kubandikwa katika vibao, ukuta wa nyumba, vitambaa, kwenye gari au chombo chochote kwa madhumuni ya kunadi biashara, huduma au bidhaa"

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Wakala" maana yake ni Taasisi, Kampuni au Asasi yoyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

Ushuru wa Matangazo

4. Halmashauri itatoza Ushuru wa matangazo yatakayotangazwa katika eneo la mamlaka ya Halmashauri kwa mujibu wa viwango vilivyotajwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Kibali cha matangazo

5. (1) Mtu yeyote, Kampuni au Taasisi kabla ya kuweka au kutangaza tangazo lolote atawajibika kuomba idhini kutoka kwa Halmashauri ambapo atajaza fomu maalum na atalipia ada ya maombi hayo;

(2) Halmashauri inaweza kukubali au kukataa maombi ya kuweka au kutangaza tangazo baada ya kujiridhisha kuwa tangazo hilo lina maudhui ambayo ni kinyume cha maadili au linavunja matakwa ya Sheria yoyote ya Nchi;

(3) Endapo Halmashauri itakataa maombi ya kuweka au kutangaza tangazo kutokana sababu zilizotajwa kwenye kifungu kidogo cha (2) hapo juu, itamtaarifu kwa maandishi Mwombaji ikimweleza sababu za kukataa maombi hayo na kumpa nafasi ya kurekebisha Tangazo lake;

(4) Kabla ya kutoa idhini ya kutangaza, Halmashauri itajiridhisha-

(a) aina ya tangazo;
(b) vipimo vya ukubwa, urefu na upana wa tangazo;
(c) mbinu zitakazotumika kutangaza; na

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

(d) Uwepo wa leseni ya biashara na/au usajiri wa biashara.

(5) Taarifa zilizowasilishwa kutokana na kifungu kidogo cha (4) hapo juu zitatumika katika kukokotoa viwango vya ada na ushuru ambao Mwombaji atatakiwa kuilipa Halmashauri.

Muda wa kibali

6. (1) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria ndogo hizi kitatumika kwa mujibu wa muda utakaotajwa katika kibali husika, na endapo kibali kitapitwa na wakati kutokana na muda wake kuisha basi Mwombaji anaweza kuomba kibali kingine;

(2) Vibali vyote vitatolewa na kusainiwa na Mkurugenzi au Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri.

Maeneo ya kutangaza

7. Halmashauri itatenga maeneo maalum kwa ajili ya kuweka mabango na kutangaza tangazo na kuainisha maeneo hayo katika kibali cha Mwombaji.

Udhibiti katika maeneo maalum

8. Halmashauri itadhibiti kwa kuzuia uwekaji mabango au kufanya matangazo katika maeneo ya maalum ili kuepusha bughudha au kero kwa Watumiaji wa maeneo hayo.

Kuondoa Bango au Tangazo

9. (1) Halmashauri inaweza kumtaka Mmiliki wa bango au tangazo kuondoa tangazo au bango husika endapo-

(a) muda wa kibali cha kutangaza umeisha;

(b) Mmiliki amekiuka masharti yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha 5(2);

(c) Mmiliki ameshindwa kulipia ada na ushuru wa bango au tangazo husika;

(d) bango au tangazo limechakaa na kuharibu

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

mandhari ya Halmashauri; au

(e) kwa sababu nyingine yoyote itakayoelezwa na Halmashauri.

(2) Endapo Mmiliki atashindwa kutekeleza matakwa ya kifungu kidogo cha (1) hapo juu, Halmashauri kwa taarifa au bila taarifa italiondoa bango au tangazo husika na inaweza kumdai Mmiliki wa bango au tangazo gharama iliyoingia katika kuondoa bango au tangazo hilo.

(3) Ni wajibu wa Mmiliki wa tangazo au bango lolote litakaloondolewa kutokana na ilani iliyotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuhakikisha jengo au eneo ambalo tangazo lake liliwekwa linabakia katika hali nzuri na salama .

Msamaha

10. Halmashauri inaweza kutoa msamaha wa kulipa ushuru wa matangazo kwa Taasisi na Idara za Serikali, Taasisi za kidini, mabango yanayohusu alama za usalama barabarani, au mabango au matangazo mengine kwa kadri itakavyoelekezwa na Halmashauri.

Marufuku

11. (1) Itakuwa ni marufuku -

(a) kuweka au kutangaza tangazo bila idhini ya Halmashauri;

(b) kuweka mabango katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(c) kuweka mabango ya aina yoyote itakayoficha au kuzuia au kusababisha alama za barabarani kutoonekana; au

(d) kuweka tangazo kwenye makutano ya barabara, kona, au mzunguko wa barabara ambalo litazuia muonekano wa Barabara.

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

Ilani

12. Ilani au Taarifa yoyote itakayotolewa na Halmashauri itaonekana imemfikia Mhusika endapo itapokelewa na Mhusika mwenyewe, Mtu yeyote anayeishi kwenye nyumba ya Mhusika wa tangazo au Msaidizi wake, Mtu yeyote aliye ajiriwa katika ofisi ya Mhusika, au imetumwa kwa njia ya posta, barua pepe, nukushi katika anwani ya mmiliki iliyopo katika kumbukumbu za Halmashauri.

Ukaguzi

13. Halmashauri inaweza kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kujiridhisha na utekelezwaji wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na Adhabu

14. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi Elfu hamsini (50,000/=), au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi anaweza kumtoza Mtu yeyote faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo Mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini na kutekeleza wajibu wake wa kulipa ushuru.

JEDWALI LA KWANZA

ADA YA MABANGO NA MATANGAZO

*(limetungwa chini ya kifungu cha 4)*

| *Na.* | *Aina ya Tangazo* | *Kiwango cha Ushuru (kwa mwaka)* |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kuweka matangazo | 3,000/= kwa kila ombi |
| 2. | Matangazo yanayong’aa *(kwa Mwaka),* | 5,000/= kwa futi ya mraba |
| 3. | Matangazo yasiyong’aa *(kwa Mwaka),* | 3,000/= kwa futi ya mraba |
| 4. | Matangazo kwenye kuta za Nyumba (yanayong’aa *(kwa Mwaka),* | 2,500/= kwa futi ya mraba |
| 5. | Matangazo kwenye kuta za Nyumba yasiyong’aa *(kwa Mwaka),* | 2,000/= kwa futi ya mraba |

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Tangazo kwa kutumia Kitambaa | 25,000/= kwa Wiki |
| 7. | Matangazo ya vipaza Sauti/ Magari na Promosheni | 50,000/= kwa kibali |
| 8. | Tangazo la umeme (trivision) | 15,000/ kwa futi mraba |

JEDWALI LA PILI

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI

*(Chini ya kifungu cha 5(1)*

SEHEMU YA KWANZA (Taarifa za Mwombaji)

1. Jina la Mwombaji/ Kampuni: ……………..……………………………….
2. Anwani ya Mwombaji; ………………….……………………
3. Aina ya tangazo ya:………………….…… .....
4. Eneo analokusudia kuweka Bango/Tangazo …………………………………………….
5. Muda wa Bango/Tangazo :……………………………………………..
6. Ukubwa wa Tangazo: …………………………………………………
7. Ada ya kibali Sh. …………………............
8. Stakabadhi ya malipo: ………………………
9. Namba ya leseni ya Biashara ………………………………………………
10. Muonekano wa tangazo **Lenye mng'aro/ lisilo na mng'aa** *(weka alama ya tiki kwa inayohusika)*
11. Sahihi:……………………………………….
12. Tarehe: ……………………………………..

SEHEMU YA PILI (Kwa Matumizi ya Ofisi)

1. Maombi Na.……………..…….……… 2. Ada ya kibali Sh:. …………...........

3. Namba ya Stakabadhi ya malipo: ……. 4. Tarehe:…………………………………..

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*weka alama ya tiki kwa inayohusika*)

Sababu:……………………………………………………………………………………………

Jina: ………………………… Saini: …………………………………
Tarehe: ………………………

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

JEDWALI LA TATU
KIBALI CHA BANGO/TANGAZO
*(Limetungwa chini ya kifungu cha 6(2)*

SEHEMU YA KWANZA: (Taarifa ya Mwenye Kibali)

1. Jina kamili la Mwombaji: ……………
2. Anuani ya Mwombaji: ………………
3. Nambari ya kiwanja na Kitalu: ………
4. Kata ya ……………………
5. Barabara/Mtaa: ………………………
6. Aina ya Bango/Tangazo: ……………
7. Ukubwa wa Bango/Tangazo;…………

SEHEMU YA PILI: (Masharti ya kibali)-

1. ………………………………………………………………………………………… ………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………… …………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………… …………………………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………………………… …………………………………………………………………………………………

Pamoja na masharti yaliyotajwa hapo juu, Halmshauri imeridhia Kibali hiki kitumike kuanzia Tarehe …………. Mwezi ………… Mwaka 20…. na ukomo wake wa kutumika ni Tarehe ………………… Mwezi ……. mwaka 20…..

Kibali hiki kimetolewa leo, Tarehe ……… Mwezi ………. Mwaka 20……… na:-

Jina kamili: ……………………………………………….………………

Cheo: …………………………..………….Saini: …………..…………….

*Tangazo la Serikali Na.20 (Linaendelea)*

JEDWALI LA NNE
FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 15)*

Mimi …………………………… wa S.L.P. …………, …………………………………. Nimekiri kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nimetenda kosa la ………………………… katika Eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, kosa ambalo ni kinyume na na kifungu cha …………….… cha Sheria ya Ndogo za (Ushuru wa Matangazo) za Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi za Mwaka 2016.
**Kwa hiyo**, Kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya Kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini:………………………………………………...

Mbele yangu:-
Jina:…………………………………………….
Saini:……………………………………………
Wadhifa: ………………………………………

Nembo ya halmashauri ya Wilaya ya Malinyi imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio la Halmashauri iliyotolewa katika kikao kilichofanyika tarehe 23.04.2016 na ilibandikwa mbele ya:-

SAID ALLY MSOMOKA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.*

FADHILI NASSORO LIGUGUDA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*